# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
## CHUO CHA UALIMU - VIKINDU

**FOMU YA MKATABA WA UJENZI KWA FUNDI**

**A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | **MWAJIRI** | Mkuu wa Chuo,<br>Chuo cha Ualimu: VIKINDU.<br>S. L. P. 16268, DAR ES SALAAM.<br>Kny:<br>Katibu Mkuu<br>Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. |
| 2 | **JINA NA ANWANI YA FUNDI (*Mwajiriwa*)** | Jina: JEREMIAH ABEL MCHOMVU<br>Anwani: S.L.P 10 MKURANGA<br>Simu: 0716207080 |
| 3 | **ENEO LA UJENZI** | ***VIKINDU TC - VIKINDU*** |
| 4 | **MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI** | ***KAZI YA UFUNDI WA UJENZI WA MADARASA MAWILI (02)*** |
| 5 | **GHARAMA YA UFUNDI (+ *Skills Development Levy*):** | **MILIONI NANE TU.**<br>**(TSH. 8,000,000.00)**<br>***(gharama ilivyo katika kipengele 3.1)*** |
| 6 | **MUDA WA MKATABA**<br>(Tangu Kusainiwa kwa Mkataba): | Tarehe ya Kusaini: 02/02/2022<br>Muda: 75 siku<br>Tarehe ya Kuanza Kazi: 07/02/2022<br>Tarehe ya Kumaliza Kazi: 23/02/2022 |
| 7 | **MASHARTI YA MALIPO:** | • Hakuna Malipo ya Awali<br>• Fundi atalipwa kwa awamu, yani baada ya kazi husika kukamilika na kukaguliwa |
| 8 | **IDADI YA MAFUNDI WASAIDIZI** | Wasiopungua wawili (2). |
| 9 | **MUDA WA KAZI KWA SIKU** | MUDA WA KUFIKA & KUANZA KAZI: Saa 1:30 Asubuhi<br>MUDA WA KUFUNGA KAZI/KUTOKA: Saa 11:00 [illegible]oni |

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

## 3: MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kulingana na maelekezo ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Mwajiri atatoa vitendea kazi vyote kama "concrete mixer", toroli, karai, ndoo, chepe, ngazi, n.k.
3. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi *(kama inavyooneshwa katika kijeduari hapa chini)* na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.

### 3.1 Jedwari la mchanganuo wa kazi ya Ujenzi

| MUAINISHO WA GHARAMA ZA KAZI ZA UASHI-JENGO JIPYA LA MADARASA MAWILI MAPYA | | |
|---|---|---|
| **SN** | **KAZI** | **GHARAMA** |
| 1.1 | Kusafisha eneo kwa kuondoa udongo wenye mboji | 50,000 |
| 1.2 | Kuchimba msingi kimo kisichozidi 750mm | 200,000 |
| 1.3 | Kuweka zege kwenye msingi | 300,000 |
| 1.4 | Kujenga ukuta wa msingi wenye unene 230mm | 500,000 |
| 1.5 | Kujaza kifusi cha morumu | 240,000 |
| 1.6 | Kufunga na kujenga ring beam ya chini na ya juu | 100,000 |
| 1.7 | Kupanga mawe, blinding na kuweka DPM | 400,000 |
| 1.8 | Kumwanga jamvi C20 ( 100MM oversite concrete) kuweka sakafu ya niru ( kioo) kumwangilia siku saba(7) | 700,000 |
| 1.9 | Kujenga ukuta wenye unene wa 150mm | 1,000,000 |
| 10 | Kufunga chuma kwenye ring beam | 150,000 |
| 11 | Kufunga form work kwenye ring beam | 120,000 |
| 12 | Kumwanga zege kwenye ring beam na kumwangilia siku saba | 300,000 |
| 13 | Kujenga kozi mbili za tofali juu ring beam | 400,000 |
| 14 | Kujenga gebo nne | 200,000 |
| 15 | Kuweka frem za madirisha na milango | 100,000 |
| 16 | Kujenga matungilizi | 150,000 |
| 17 | Kupiga plasta ndani na nje | 400,000 |
| 18 | Kujenga ngazi | 100,000 |
| 19 | Kuweka /kujenga vigae na terazzo | 460,000 |
| 20 | Kusafisha mazingira ya ndani na nje baada ya ujenzi kukamilika | 50,000 |
| 21 | Skimmimg na kupaka rangi ndani na nje | 550,000 |
| | **JUMLA** | **6,470,000.00** |

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

| SN | MUAINISHO WA GHARAMA ZA KAZI ZA KUPAUA -JENGO JIPYA LA MADARAS MAWILI | |
|---|---|---|
| | KAZI | GHARAMA |
| 1.1 | Kupaua madarasa mawili mapya kama inavyoonekana kwenye ramani, kutengeneza kench,kuweka bati,fisha bodi pamoja na mifereji/migongo ya bati na gutter | 860,000 |
| 1.2 | Kupiga brandaring, gypsum bodi pamoja na mikanda yake | 2[illegible],000 |
| | JUMLA | 1,110,000 |

| MUAINISHO WA GHARAMA ZA KAZI ZA UMEME-MAJENGO MAPYA YA CHUO | | |
|---|---|---|
| SN | KAZI | GHARAMA |
| 1. | Kufanya wiring jingo zima | 200,000 |
| 2. | Kufunga umeme | 120,000 |
| 3. | Kufunga taa, switch, socket, main switch, circuit bracker, feni na kila kinachohitajika kwenye jingo. Kuhakikisha kuwa mfumo mzima wa umeme unafanya kazi vizuri | 100,000 |
| | JUMLA | 420,000.00 |
| | JUMLA KUU | 8,000,000.00 |

4. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.

5. Fundi atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.

6. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.

7. Fundi atahusika na vitendo *(kama wizi, uharibifu wa mali za chuo)* vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.

8. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.

9. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Mwezi mmoja baada ya kazi kukamilika *(Retention Money)* na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

10. Ucheleweshaji wa Kazi:

- Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.

11. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

- Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri *(kutokana na fedha au vifaa)*, Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kazi.

12. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.

13. Maelekezo ya kazi yatatolewa na Msimamizi Mkuu wa Kazi (Clerk of Works) na mwajiriwa (Fundi) ataomba malipo fedha kwa kazi aliyoifanya kwa mkuu wa Chuo kupitia Msimamizi wa Kazi na atalipwa endapo ukubwa wa kazi aliyofanya itakaguliwa na kufika angalau 30%.

**MWAJIRI:**

Saini: ............

Jina: AMINA N. TOU

Cheo: MKUU WA CHUO

Tarehe: 02/02/2022

**SHAHIDI WA MWAJIRI**

Saini: ............

Jina: SAIA CHARLES

Cheo: MKUFUNZI

Tarehe: 02/02/2022

**FUNDI:**

Saini: ............

Jina: JEREMIAH ABEL MCHOMVU

Cheo: FUNDI MKUU

Tarehe: 2/02/2022

**SHAHIDI WA FUNDI**

Saini............

Jina: ............

Cheo:............

Tarehe: 02/02/2022

Principal
Vikindu Teachers' College
P. O Box 1626
DAR ES SALAAM

Scanned with CamScanner